PRESS RELEASE

PR 24/378

# Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Lafikia Makubaliano ya Ngazi ya Wafanyakazi na Serikali Kuhusu Mapitio ya Nne ya Mpango wa Ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility) na Mapitio ya kwanza ya Mpango wa Mageuzi kwa ajili ya kushughulikia Changamoto za Mabadiriko ya Tabia ya Nchi (Resilience and Sustainability Facility)

**FOR IMMEDIATE RELEASE**

Taarifa kwa vyombo vya habari mwishoni mwa ziara ya Wafanyakazi kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ambayo inawasilisha matokeo ya awali baada ya kutembelea nchi. Maoni yaliyotolewa katika taarifa hii ni ya wafanyakazi wa IMF na si lazima yawakilishe maoni ya Bodi Tendaji ya IMF. Kulingana na matokeo ya awali ya kazi yao, wafanyakazi watatayarisha ripoti ambayo, kwa kutegemea idhini ya uongozi wa shirika, itawasilishwa kwa Bodi Tendaji ya IMF kwa ajili ya majadiliano na uamuzi.

- *Serikali ya Tanzania imefikia makubaliano ya ngazi ya wafanyakazi na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kuhusu mapitio ya nne ya mpango wa ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility) na mapitio ya kwanza ya mpango wa mageuzi ya kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia ya nchi RSF (Resilience and Sustainability Facility).*
- *Kasi ya ukuaji wa uchumi inaongezeka mwaka 2024 kutokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia na mapato na matumizi ya serikali na mfumuko wa bei kuwa chini. Vipaumbele vya sera vinaendelea kuangaziwa katika kuruhusu viwango vya kubadilisha fedha za kigeni kuendana na nguvu ya soko, kuboresha mfumo wa sera ya fedha, kuendeleza juhudi za kubana matumizi ya serikali bila kuathiri ukuaji wa uchumi, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, na kuharakisha utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo.*
- *RSF inaunga mkono juhudi za serikali za kuendeleza mageuzi ya kimuundo na uwekezaji katika kukabiliana na hatari na changamoto za mabadiliko ya tabia ya nchi.*

**Washington, DC- 17 Oktoba 2024:** Wafanyakazi kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wakiongozwa na mkuu wa ujumbe huo kwa Tanzania, Bwana Charalambos Tsangarides walifanya ziara mjini Dodoma na Dar es Salaam kuanzia tarehe 2 hadi 17 Oktoba, 2024 ili kufanya majadiliano kuhusu mapitio ya 4 ya utekelezaji wa mpango wa ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility) na mapitio ya kwanza ya mpango wa mageuzi kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zitokanazo na mabadiliko ya tabia ya nchi RSF (Resilience and Sustainability Facility). Endapo matokeo ya mapitio haya yataidhinishwa na Bodi Tendaji ya IMF, serikali itapokea kiasi cha SDR milioni 198.61 (takribani dola za marekani milioni 265.78) na hivyo kufikisha jumla ya kiasi cha SDR milioni 568.84 (takribani dola za marekani milioni 758.11) zilizokwishatolewa na IMF chini ya mpango wa ECF na kiasi cha SDR milioni 85.24 (takribani dola za marekani milioni 114.07) chini ya mpango wa RSF.

Mwishoni mwa ziara, Bwana Tsangarides, ametoa taarifa ifuatayo:

“Ninayo furaha kutangaza kwamba Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) limefikia makubaliano ya ngazi ya wafanyakazi na serikali ya Tanzania kuhusu sera zinazohitajika ili kukamilisha mapitio ya nne chini ya mpango wa ukopeshaji kwa Tanzania unaoungwa mkono na ECF, na mapitio ya kwanza ya mpango wa RSF. Bodi Tendaji ya IMF itajadili maombi haya katika wiki zijazo.

“Kasi ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania mwaka 2024 inaendelea kuimarika kutokana na shughuli za kiuchumi kukua kwa takriban asilimia 5.4 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024 baada ya ukuaji wa mwaka wa asilimia 5.1 mwaka 2023. Mfumuko wa bei kwa mwezi Septemba ulibakia kuwa asilimia 3.1 (mwaka kwa mwaka), kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la Benki Kuu ya Tanzania. Mitikisiko ya kiuchumi ya hapo awali imepungua, na kuongezeka kwa fedha za kigeni kwenye uchumi kumepunguza kiasi uhaba wa fedha za kigeni katika soko rasmi la fedha hizo, ingawa bado tatizo halijaisha. Matarajio kuhusu uchumi ni mazuri huku ukuaji ukitarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.4 mwaka 2024; hata hivyo, viashiria hatarishi vya ukuaji wa uchumi vinaweza kutokana na kuongezeka kwa migogoro ya kikanda, kubadirika kwa bei za bidhaa, kushuka kwa uchumi wa dunia, kuibuka tena kwa upungufu wa fedha za kigeni katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025, na majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, vyote hivi vinaweza kusababisha athari mbaya kwa uchumi.

“Nakisi ya mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliimarika hadi kufikia takriban asilimia 3.1 ya Pato la Taifa mwaka wa fedha 2023/24 kutoka asilimia 6.5 ya Pato la Taifa mwaka uliopita, kutokana na ukuaji mkubwa wa mauzo ya huduma nje ya nchi na kushuka kwa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kusaidiwa na kushuka kwa bei za bidhaa. Kuimarika kwa nakisi ya mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma nje ya nchi (mwaka kwa mwaka), kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kwa asilimia 13 dhidi ya dola ya marekani, na mapato ya msimu ya dola katika nusu ya pili ya mwaka yamesaidia kupunguza kiasi tatizo la soko la fedha za kigeni. Benki Kuu ya Tanzania imesisitiza dhamira yake ya kuruhusu mabadiliko zaidi kwenye viwango vya kubadilisha fedha za kigeni na kuhakikisha viwango hivyo vinaamuliwa na nguvu ya soko, huku ikihakikisha inaingia tu kwenye soko pale inapojitokeza hali mbaya ya soko, kulingana na sera yake ya uingiaji sokoni. Kuendeleza sera ya fedha ya kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi kutasaidia pia juhudi za kupunguza shinikizo katika soko la fedha za kigeni na kuleta utulivu wa bei za bidhaa na huduma.

“Serikali ilfanikiwa kutekeleza mpango wake wa kubana matumizi Mwaka wa Fedha 2023/24 kupitia uboreshaji wa makusanyo ya mapato ya kodi na marekebisho katika matumizi ya kawaida. Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/25 inalenga kubana matumizi bila kuathiri ukuaji wa uchumi ikiungwa mkono na sera ya kodi na juhudi za usimamizi wa mapato. Serikali imesisitiza dhamira yake ya kuongeza matumizi kwenye huduma za kijamii ili kuwalinda walio hatarini.zaidi. Mpango wa serikali wa mageuzi ya kimuundo unalenga kusaidia ukuaji wa uchumi thabiti, endelevu, na jumuishi unaotokana na kuboreshwa kwa mazingira ya kufanya biashara na utawala bora.

“Katika kikao chake cha mwezi Oktoba, Kamati ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania ilibakiza riba ya Benki Kuu kwenye kiwango kilichokuwepo hapo awali cha asilimia 6, ili kuendelea kudhibiti viashiria vya kuongezeka kwa mfumuko wa bei. Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kurekebisha sera yake ya fedha ili kudumisha utulivu wa bei za bidhaa na huduma,

huku ikilinda ufufukaji wa shughuli za kiuchumi kutokana na athari za mtikisiko wa uchumi wa dunia na hali mbaya ya hewa.

“Ikiungwa mkono na mpango na RSF, serikali inatekeleza mpango wa mageuzi yanayohusu mabadiliko ya tabianchi ili kutatua changamoto za kisera ili kuimarisha uthabiti wa uchumi wa Tanzania. Juhudi zinaendelea kufafanua kwa uwazi mfumo wa kitaasisi wa sera zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha usimamizi wa uwekezaji wa umma kulingana na athari na hatari za mabadiliko ya tabia ya nchi. Utekelezaji wa mageuzi yaliyomo kwenye mpango wa RSF unaendelea, na serikali inaendelea kukusanya usaidizi wa kiufundi na kifedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

"Ujumbe kutoka IMF ulikutana na Waziri wa Fedha, Mhe. Dr. Mwigulu Nchemba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bwana Emmanuel Tutuba, viongozi wengine waandamizi wa serikali, washirika wa maendeleo, na wawakilishi wa sekta binafsi. Wajumbe kutoka IMF wanapenda kuzishukuru mamlaka za Tanzania pamoja na washirika wengine kwa ukarimu wao, na majadiliano ya wazi na yenye tija”